ISSN 0856-0323

MWAKA WA 71,
TOLEO NA. 49

GAZETI

23 Novemba, 1990

BEI SH. 10/- LA DAR ES SALAAM

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na
Kuandikishwa Posta kama
Gazeti

YALIYOMO

	Taarifa ya Kawaida	Uk.
Notice *re* Supplements	Na. 806	441
Tanzia		441
Baraza la Sanaa la Taifa	Na. 807	441
Muunganisho wa Wadhamini	Na. 808	441
Mtumizi wa Alama za Biashara	Na. 809	442
Kampuni iliyofutwa katika Daftari la Makampuni	Na. 810	442
Uvumbuzi Usiigwe	Na. 811-2	442
Uthibitisho na Usimamizi wa Mirathi	Na. 813-20	442/44

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 806

Notice is hereby given that By-laws, and Notices as set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 44 dated 23rd November, 1990 to this number of the *Gazette*:—

The Babati District Council (Prevention of Soil Erosion and Water Conservation) By-laws, 1990 (Government Notice No. 485 of 1990).

Tangazo la Magereza (Uteuzi wa Wakaguzi wa Magereza Mkoa wa Tanga) la Mwaka, 1990 (Tangazo la Serikali Na. 486 la Mwaka 1990).

Tangazo la Magereza (Uteuzi wa Wakaguzi wa Magereza Mkoa wa Shinyanga) la Mwaka 1989 (Tangazo la Serikali Na. 487 la Mwaka, 1990).

TANZIA

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Nd. Mwajuma Salum, Koplo wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 2/10/1990.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 807

SHERIA YA BARAZA LA SANAA LA TAIFA NA. 23 YA 1984

Kwa mujibu wa kifungu cha I cha Sheria Na. 23 ya 1984 Waziri wa Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii anatangaza kwamba Sheria Na. 23 ya 1984 imeanza kutumika tarehe 1 Desemba, 1986.

A. M. VUAI,
Katibu Mkuu
Wizara ya Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 808

MUUNGANISHO WA WADHAMINI
Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini
(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa ya kuwa kufuatana na kifungu 3(1) cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inatolewa Shahada ya Muunganisho wa Wadhamini kwa jina lifuatalo:—

THE REGISTERED TRUSTEES OF ZAWIYA EL QADIRIYA, MWANZA.

Dar es Salaam,
12 Novemba, 1990

G. J. NGOTOLAINYO,
Kaimu Msimamizi Mkuu wa Wadhamini

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika *Gazeti*. Yapelekwe kwa **Mhariri, Idara Kuu ya Utumishi—Ofisi ya Rais, S.L.P. 2483, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 20781/4.** *Kabla ya Jumamosi ya kila Juma.*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 809

SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ALAMA ZA BIASHARA

(Sura ya 394)

TANGAZO linatolewa kwamba mtumizi wa alama za biashara zilizotajwa hapo chini ameandikishwa katika daftari la Alama za biashara kama ifuatavyo:—

Jina la Mwenyemali: Religious Technology Center.

Anuani: 1710 Ivar Avenue, City of Los Angeles, State of California, United States of America.

Anuani ya Utumishi: Donaldson & Wood Mawakili S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Jina la Mtumiaji: New Era Publication International Aps.

Anuani: Store Kongensgade 55, 1264 Copenhagen K, Denmark.

Alama za biashara na Bidhaa zake: 19310, 19345, 20058, 20621, 19309, 19341 na 19340.

Masharti: Kama yalivyo katika tamko la kisheria la tarehe 21 Agosti, 1990.

T. S. D. MTETEWAUNGA,
Msajili Msaidizi Mwandamizi
wa Alama za Biashara

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 810

SHERIA YA MAKAMPUNI

(Sura ya 212)

Kampuni Iliyofutwa katika Daftari la Makampuni

Inatolewa ilani chini ya kifungu 283 (5) cha sheria ya Makampuni kwamba kampuni ifuatayo imefutwa katika daftari la Makampuni.

1. KILIMANJARO HOTELS LIMITED

Dar es Salaam,
22 Oktoba, 1990.

L. KISHEBUKA (BIBI),
Msajili Msaidizi wa Makampuni

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 811

SHERIA YA UANDIKISHAJI

Uvumbuzi Usiigwe

(Sura ya 217)

Inatangazwa kwa watu wote kwamba Hati za Uvumbuzi zenye maelezo yaliyomo kwenye nyongeza ya Tangazo hili ziliandikwa kuwa Namba 2405 ya 1990 katika Daftari la Tanganyika la kuandikisha hati za Uvumbuzi mnamo tarehe 5 mwezi wa Juni, 1990.

NYONGEZA

Nambari ya Ombi: 2405
Tarehe ya Ombi: 5/6/1990
Jina la Mwombaji: GLAXO SPA
Anuani iliyoandikishwa: Via A Fleming 2 Verona Italy.

Maelezo ya kukubaliwa katika Ulaya ya Uingereza: Hati ya maainisho No. 2181127 ya tarehe 20/8/1986 iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza.

Aina ya Kitu Kilichovumbuliwa: 4-Phenyl-Dihydropridine Carboxylic Acid Derivatives.

Hati n.k. zilizowasilishwa kwenye masjala: 1. hati ya maainisho ya Uvumbuzi iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza.
2. Hati ya Msimamizi Mkuu wa Uvumbuzi wa Ulaya ya Uingereza.
3. Hati ya Mwakilishi Donaldson & Wood, Advocated, P.O. Box 176, Dar es Salaam.

S. D. MTETEWAUNGA,
Msajili Msaidizi wa Uvumbuzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 812

SHERIA YA UANDIKISHAJI

Uvumbuzi Usiigwe

(Sura ya 217)

Inatangazwa kwa watu wote kwamba hati za Uvumbuzi zenye maelezo yaliyomo kwenye nyongeza ya Tangazo hili ziliandikwa kuwa Namba 2415 ya 1990 katika Daftari la Tanganyika la kuandikisha Hati za Uvumbuzi mnamo tarehe 11 mwezi wa Sepetemba, 1990.

NYONGEZA

Nambari ya Ombi: 2415
Tarehe: 11/9/1990
Jina la Mwombaji: CIBA GEIGY Ag.
Anuani iliyoandikishwa: Klybeckstrass 141,4002 Basle Switzerland.

Maelezo ya kukubaliwa katika Ulaya ya Uingereza: Hati ya maainisho ya uvumbuzi No. 0084020 iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza tarehe 5 January, 1983.

Aina ya kitu kilichovumbuliwa: N-Aryisulfonyl-N'-Pyrimidinyl Urea.

Hati n.k. zilizowasilishwa kwenye masjala: 1. Hati ya maainisho ya uvumbuzi iliyoandikishwa ulaya ya Uingereza.
2. Hati ya Msimamizi Mkuu wa Uvumbuzi Ulaya ya Uingereza.
3. Hati ya Mwakilishi Donaldosn & Wood, Advocates, P.O. Box 176, Dar es Salaam.

J. S. THOBIAS,
Msajili Msaidizi wa Uvumbuzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 813

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Mbeya)

SHAURI LA MIRATHI NA. 6 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya

Lebi Mwanjoka, Marehemu wa Mbeya

na

Richard Lebi Mwanjoka, Mwombaji wa Mbeya

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kibali cha usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5 mwezi wa Desemba, mwaka 1990.

Imewasilishwa Mbeya leo tarehe 4 Oktoba, 1990.

.....,
Ag. Msajili wa Wilaya, Mbeya

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 814

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 201 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya

Victor Chiuja, Marehemu

na

Stella Chiuja, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/barua za usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 7 mwezi wa Januari, mwaka 1991.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo hii tarehe 7 mwezi Novemba, 1990.

.....,
Hakimu Mkazi Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 815

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 75 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya

Shabani Ali, Marehemu

na

Mwajuma Shabani, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri hayo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5 mwezi wa Desemba, mwaka 1990.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 5 Septemba, 1990.

.....,
Hakimu Mkazi, Dar es Salaam

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 816

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbeya)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 5 LA MWAKA 1990

Maombi ya Usimamizi wa Mirathi ya

Kabirdin Kassam Nurmohamed, Marehemu

na

Mrs. Gulshan Kabirdin Kassam Nurmohamed, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu ambaye ametajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla kya kutolewa kibali cha usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yamewakilishwa mnamo au kabla ya tarehe 8 Desemba, 1990.

Imewasilishwa Mbeya leo tarehe 8 Novemba, 1990.

M. M. P. MUTONGORE,
Ag. Msajili wa Wilaya, Mbeya

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 817

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi—Kisutu, D'Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 108 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya

Halima Simba, Marehemu

na

Ramadhani Haruna, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 2 mwezi Januari, 1990.

Hakimu Mkuu Mkazi
D'Salaam

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 818

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi—Kisutu, D'Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 109 LA MWAKA 1990

Maombi ya Usimamizi wa Mirathi ya

Ramadhani Farahani, Marehemu

na

Ramadhani Haruna, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 2 mwezi Januari, 1991.

Hakimu Mkuu Mkazi,
D'Salaam

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 819

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 77 LA MWAKA 1990

Maombi ya Barua za Usimamiaji wa Mirathi ya

Safina Bint Mirando, Marehemu

na

Kondo Hamisi Hassan Madamakuru, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/Barua za Usimamiaji wa Mirathi kwa waombaji waliyotajwa hapo juu/ kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kablá ya tarehe 20 mwezi wa Novemba, mwaka 1990.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 1 mwezi Oktoba, 1990.

.....

Naibu Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 820

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, D'Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 97 LA MWAKA 1990

Maombi Barua za Usimamiaji wa Mirathi ya

Velabai Laxmidas Bhanji, Marehemu

na

Madhursinh Laxmidas Bhanji, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/Barua za Usimamiaji wa Mirathi kwa waombaji waliyotajwa hapo juu/ kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 mwezi wa Desemba, mwaka 1990.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 12 mwezi Novemba, 1990.

Naibu Msajili

SAHIHISHO

Kuhusu TAARIFA YA KAWAIDA NA. 701 la Gazeti la Serikali la tarehe 19 Oktoba, 1990.

Jina la Mwakilishaji wa alama ya Biashara nambari 21351 na 21352 *isomeke* STANLEY & MACKENZIE na sio SPOOR & MACKENZIE.

Toleo Na. 42 la Gazeti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la tarehe 13/10/1989, Taarifa ya Kawaida Na. 769, Aya ya 4, futa kumbukumbu zote za mtahiniwa HK 8009 JOSEPH A. MWAKIPESILE, Tech., P.O. Box 762, (Mbeya) kisha mwongeze mtahiniwa huyu katika aya ya 3 kuonyesha kuwa sasa amefaulu mtihani wote wa Kiswahili Kigumu. (Kuandika na Kusoma) baada ya kufanya na kufaulu masomo aliyoshindwa hapo awali.

Limepigwa Chapa na Mpigachapa wa Serikali, Dar es Salaam—Tanzania